Northern Territory Office of the Public Guardian

Fact sheet

# Kuelewa Sheria ya Ulezi ya NT ya Watu Wazima

Karatasi ya ukweli (Swahili)

## Katika karatasi hii ya ukweli

*Sheria ya Ulezi ya NT ya Watu Wazima ya 2016* (*Guardianship of Adults Act 2016*) ilianza kutumika tangu tarehe 28 Julai 2016. Hii karatasi ya ukweli inaelezea:

| | |
|---|---|
| Jinsi sheria inafanya kazi | Maelezo ya jumla na majukumu ya Ulezi wa Umma na NTCAT |
| Inajumuisha nini | Kufanya maamuzi kulingana na kanuni za ulezi |
| Kuna amri ngapi hapo | Amri ya muda mfupi na ya mikoani, na zile za vijana |

## Sheria inafanya kazi namna gani?

### Maelezo ya jumla ya Sheria ya Ulezi

Sheria ya Ulezi inasaidia watu wasio na uwezo wa kufanya maamuzi ambao wanahitaji msaada wa kufanya maamuzi kuhusu masuala yao binafsi au ya kifedha.

Inashughulikia watu wenye uharibifu wa utambuzi kutokana na sababu yoyote, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa akili, matatizo akili, ulemavu wa akili au uharibifu wa ubongo.

Sheria ya Ulezi hutambua ustawi wa jumla wa watu wazima, haki za binadamu na uhuru wa msingi, na inaunganisha Mkoa wa Kaskazini na Mkataba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Watu wenye ulemavu.

Sheria ya ulezi:

- kuanzisha ofisi huru ya Ulezi wa Umma na afisa huru wa kisheria kama Mlezi wa Umma
- kuanzisha kanuni za uhifadhi kamili
- kuhamishwa mamlaka kutoka kwa Mahakama ya Mitaa kwenda Mahakama ya kiraia na utawala (NTCAT) ya Mkoa wa Kaskazini.

### Kazi ya Mlezi wa Jamii

Afisa wa kisheria wa kujitegemea anayejulikana kama 'Mlezi wa Umma' anayesimamia uangalizi katika Mkoa wa Kaskazini.

Mlezi wa Jamii:

- hutoa habari kwa walezi na watu wanaofikiria kuhusu ulezi
- inakuza upatikanaji wa huduma kwa watu wazima, wasaidizi na familia
- hufanya kama mlezi kwa mtu mzima wakati amechaguliwa na NTCAT
- hufanya utafiti na husaidia kuwaelimisha watu kuhusu ulezi
- inachunguza mambo ya ulezi.

ℹ Sheria ya Ulezi inaweka wazi uwezo wa Mlezi wa Umma na majukumu yake.

### Kazi ya NTCAT

Mamlaka ya ulezi imehama kutoka kwa Mahakama ya Mitaa hadi NTCAT. Hii inamaanisha maombi ya ulezi ('utaratibu wa ulezi') sasa unaenda kwa NTCAT kuamuliwa.

NTCAT itafanya utaratibu wa ulezi unaofaa zaidi na hali ya watu wazima. Utaratibu utasema mambo ya kibinafsi au ya kifedha ambayo mlezi ana mamlaka nayo, na mapungufu yoyote.

ℹ Tafadhali tembelea www.ntcat.nt.gov.au kujua Zaidi juu ya kuomba, kutoa au kupitia upya amri ya ulezi.

NTCAT inaweza kuchagua mlezi mmoja au Zaidi wa mtu mzima. Mlezi anaweza kuwa:

- Mlezi wa Umma
- mwenye dhamana wa jamii (kwa masuala ya fedha)
- mtu mzima anayestahili wa miaka 18 au zaidi
- muunganiko wa vyote.

© Office of the Public Guardian, 2018

## Sheria inajumuisha nini?

### Kanuni za Ulezi

Kanuni za ulezi hutoa mfumo wa kufanya maamuzi ambayo watetezi wote wanapaswa kufuata. Wanasema kuwa mlezi lazima daima:

- kutenda katika 'maslahi bora' ya watu wazima
- kutekeleza mamlaka yao kwa njia ambayo haizuii uhuru wa watu wazima wa uamuzi na utekelezaji
- fikiria maoni na matakwa ya sasa ya watu wazima
- wasaidie watu wazima kufanya maamuzi yao wenyewe iwezekanavyo.

Mlezi lazima atende kulingana na utaratibu wa utunzaji, Sheria ya Ulezi na amri nyingine yoyote ya NTCAT.

ℹ Tafadhali angalia sehemu ya 4 ya Sheria kwa orodha ya kina ya kanuni za ulezi.

### Mamlaka ya maamuzi ya huduma za afya

Mlezi anaweza kupewa mamlaka kwa maamuzi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maamuzi ya huduma za afya, kwa watu wazima wanao wawakilisha.

Sheria inafafanua huduma za afya kwa ujumla. Walezi wenye mamlaka ya huduma za afya wanaweza kwa ujumla kukubaliana na matibabu:

- kuhusisha ganzi ya ujumla, inayofanana au kutoa dawa anayothiri mfumo mkuu wa neva
- anahitaji daktari au mganga wa meno kufanya au kusimamia
- anahitaji kuandikiwa dawa
- ni ya kuendelea, mara kwa mara au sehemu ya mpango wa matibabu.

### Vikwazo vya maamuzi ya huduma za afya

Baadhi ya maamuzi ya huduma za afya yanaweza tu kufanywa na NTCAT. Tunaita maamuzi haya ya 'vikwazo' ya afya. Yanajumuisha:

- vitendo vinavyosababishwa na uharibifu
- kutoa mimba
- kuondoa tishu ambazo hazitakua tena kwa ajili ya kupandikiza mtu mwingine
- huduma za afya kwa utafiti wa matibabu
- huduma yoyote ya afya ambayo kanuni inasema ni vikwazo.

ℹ Tazama sehemu ya 8 ya Sheria ya Ulezi (maamuzi ya ulezi wa afya yenye vikwazo).

ℹ Tazama sehemu ya 4 ya *Sheria ya Kupandikiza na na Mwili wa Mtu ya 2011* (kuto-kuzalisha tishu).

### Mipango Binafsi ya Mapema

Mipangilio ya kibinafsi ya mapema inaruhusu mtu kupanga kwa siku zijazo ambako afya zao, kifedha na matakwa ya maisha husikika na kuheshimiwa ikiwa amepoteza uwezo wa kufanya maamuzi.

*Sheria Maalumu ya Mipango Binafsi ya 2013* (*Advance Personal Planning Act 2013*) imesasishwa ili kuifatanisha na Sheria ya Ulezi.

ℹ Tafadhali angalia 'Mipango ya kibinafsi maalumu na ulezi wa watu wazima' au tembelea www.advancepersonalplanning.nt.gov.au.

## Kuna aina ngapi za amri?

### Amri za mda mfupi (haraka) za ulezi

NTCAT inaweza kufanya amri ya muda mfupi wakati inapoamua maombi ikiwa inaaminika kuwa mtu mzima hana uwezo wa kufanya maamuzi na anahitaji mlezi haraka.

### Amri za Ulezi za mikoani

Sheria inaruhusu NTCAT kuandikisha amri za udhibiti wa ndani. Hii inatoa haja ya kuomba ulezi katika eneo la mkoa wa kaskazini wakati amri bado inatumika katika mamlaka nyingine ya Australia.

### Amri za Ulezi kwa vijana

NTCAT inaweza kufanya amri ya ulezi ya mwenye umri wa miaka 17 kwa ajiri ya wakati wa wakitimiza 18. Lengo ni kurahisisha uhamisho wa mamlaka ya uamuzi kutoka utoto hadi utu uzima.

## Nyaraka muhimu

- *Sheria ya Ulezi ya NT ya Watu Wazima ya 2016*
- *Sheria Maalumu ya Mipango Binafsi ya 2013*
- *Sheria ya Kupandikiza na na Mwili wa Mtu ya 2011*
- Mwongozo wetu wa uelewaji wa ulezi

Kama una swali lolote, tafadhali wasiliana nasi:

**1800 810 979**

public.guardian@nt.gov.au

www.publicguardian.nt.gov.au